

NAZI NA ZAKA



Na Avehei M.,
umri miaka 11,
Tahiti, French
Polynesia


Mambo! Jina langu ni Avehei. Ninaishi Tahiti. Kwenye kisiwa changu, ninapenda kuwa nje ya nyumba. Napenda kupanda milima na kuogelea katika mto au baharini. Ninapenda pia kufanya mambo pamoja na familia yangu. Ninapenda kupika, kucheza karata na kutembea kupanda milima. Ninapenda kucheza mpira na kaka yangu na binamu zangu.

Wakati wa likizo ya msimu wa kiangazi, ninafanya kazi pamoja na kaka yangu katika kijisitu cha minazi. Tunaokota nazi na kuziweka katika rundo kubwa. Pia tunakusanya majani yaliyodondoka ili kijisitu kibakie safi.

Baba wa babu yangu hutulipa tunapofanya kazi katika kijisitu hicho. Daima ninalipa zaka kwa pesa ninayolipwa. Nimejifunza kutoka kwa familia yangu na walimu wa Msingi namna ya kulipa zaka.

Ninalipa zaka kwa sababu ninajua kwamba mimi na familia yangu tunabarikiwa wakati tunapotii. Nimebarikiwa kwa familia yangu, nyumba na ulimwengu mzuri unaonizunguka.

Ninajua kwamba Mungu yu hai na kwamba ananipenda. Ninamshukuru Baba wa Mbinguni kwa familia ambayo Yeye amenipa. ●



ZAKA NI NINI?

Waumini wa Kanisa hutoa moja ya kumi ya kipato chao kwa Kanisa la Mungu. Pesa yetu ya zaka inasaidia katika ujenzi wa mahekalu na majengo ya makanisa na inawasaidia watu wenye shida. Kulipa zaka ni njia mojawapo ya kushiriki baraka zetu na watu wengine. Mungu alitupatia amri hii miaka mingi iliyopita, wakati wa Agano la Kale (ona Mwanzo 14:18-20). Kulipa zaka ni njia ya kuonesha upendo wetu kwa Baba wa Mbinguni.

